



Research Article



Check for updates

Section: Languages



This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in African Languages*, Volume 2, Issue 1, 2021



Article Information

Submitted: 20th Nov 2020
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 4th April 2021

Additional information is available at the end of the article

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online, please scan this QR code



Perspective comparison of structures and themes of two ancient epic poems and Muyaka's poems

Jessee Murithi¹ & Mwanzu Daniel Misigo²

^{1,2}Department of Literature, Linguistics and Foreign Languages, Kenyatta University, Kenya
Correspondence: murithijj2015@gmail.com

Abstract

Literature explains about events and occurrences of a particular society. The Works of literature copy structures, styles and themes from other literary Works written before them. In this perspective, this journal aims at comparing structures and themes between two ancient epic poems and poems written by Muyaka. This ancient epic poems are: *Utendi wa Al-Inkishafi* and *Liyongo*. Through this analysis we would establish if there are similar and different structural and themal characteristics between Muyaka's poems and the two ancient epic poems given that they were composed at the same period. This analysis was led by the theory of classicism. The tenets of this theory are: ancient terminologies, high level of creativity, quoting writers who wrote in different time periods among many others. According to the theory of classicism, the works of literature were measured based on other literary works. This measurement brought about rules and regulations that identified good composition of literary works. On the other hand, epic poems that were discussed in this journal are in the book of *Tenzi za Kale* that was edited.

Keywords: epic, literature, poems, themes, structure, classicism

Public Interest Statement

This research aims at comparing and contrasting the themes and structures of Muyaka's poems and ancient epic poems. The ancient poems are: *Utenzi wa Liyongo* and *Al-Inkishafi*. The question is why did Muyaka choose to be different from the rest of the poem composers who lived in his era? Why did Muyaka not follow the rules and regulations stated in the theory of classicism?

How to Cite:

Murithi, J., & Misigo, M. D. (2021). Perspective comparison of structures and themes of two ancient epic poems and Muyaka's poems. *Research Journal in African Languages*, 2(1). Retrieved from <https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/581>



© 2021 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.



Research Article

Section: Languages



Check for updates



This article is published by Royallite Global, Kenya in the *Research Journal in African Languages*, Volume 2, Issue 1, 2021

Article Information

Submitted: 20th Nov 2020
Accepted: 30th Mar 2021
Published: 4th April 2021

Additional information is available at the end of the article

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>

To read the paper online, please scan this QR code



Mtazamo linganishi wa muundo na maudhui ya tenzi mbili za kale na ushairi wa muyaka

Jessee Murithi na Mwanzu Daniel Misigo

Correspondence: murithijj2015@gmail.com

Ikisiri

Fasihi huelezea kuhusu matukio katika jamii. Kazi hizi huweza kuiga miundo, mitindo na maudhui ya kazi za awali. Kuiga huku huweza kufanya kazi hizo kuwa na vipengele vinavyofanana na kazi zilizotangulia. Kwa mkabala huu, makala hii inalenga kulinganisha miundo na maudhui ya tenzi mbili za kale za lugha ya Kiswahili ushairi wa Muyaka Tenzi hizi ni: Utendi Al-Inkishafi na Liyongo. Uchanganuzi huu utabaini ikiwa kuna sifa za kimuundo na kimaudhui zinazofanana katika tenzi hizi na pia kutofautiana hasa ikizingatiwa kuwa watunzi wa tenzi hizi walitunga katika kipindi kimoja na Muyaka. Nadharia iliyoongoza uchanganuzi huu ni nadharia ya “Ukae” (Classicism) ambayo ina mihimili kama ukale wa msamiati, ubunifu wa kiwango cha juu, kurejelewa na wasanii wengine katika enzi tofauti kati ya mingine. Kulingana na urasimi mkongwe, kazi za fasihi zilipimwa kwa misingi ya kazi nyinginezo. Upimaji huu ulibuni sheria na kanuni za utunzi bora. Aidha, tenzi zilizoshughulikiwa zimo katika kitabu cha Tenzi Tatu za Kale iliyohaririwa na Mulokozi (1999)

Maneno ya kimsingi: fasihi, ushairi, miundo, maudhui, ukae, tenzi



1.0 Utangulizi

Tenzi mbili zinazohakikiwa hapa: *Al- Inkishafi* na *Liyongo* kwa upande mmoja na kazi ya ushairi wa ki-tarbia wake Muyaka Bin Haji au Muyaka wa Muhaji (1776-1840), ni tungo zenye kudhihirisha ukale kwa sifa kadhaa. Kuna ushahidi unaoonyesha kuwa maudhui ya tenzi na ushairi wa aina ya tarbia yanatofautiana na kufanana kidogo pia, hasa kwa mujibu wa tenzi hizi mbili na ushairi wake Muyaka Bin Haji. Makala haya yanalenga kudhihirisha hoja hii. Msingi wa kanuni zitakazofafanuliwa humu ni nadharia ya “Ukae” (Classicism) ambayo ina mihimili ifuatayo:

- Ukale wa msamiati
- Ubunifu wa kiwango cha juu
- Kupendwa na umma
- Umaarufu unaotambulika na kizazi hadi kizazi
- Kurejelewa na wasanii wengine katika enzi tofauti
- Kuigizwa ama kuigwa kwa mbinu tofauti kutokana na thamani na uzuri wake.

Makala haya yameangazia miundo na maudhui yanayopatikana katika tenzi za *Liyongo* (Karne 12-13 na *Al-Inkishafi* (1810-1820). Miundo inayofafanuliwa ni kama vile: mianzo ya utenzi, mwendelezo wa hadithi, mbinu za kimazungumzo na hitimisho la utenzi, idadi ya mishororo na urari wa vina na mizani. Vile vile, usawa na utofauti wa kimaudhui utagusiwa kwa kulinganisha maudhui ya tenzi mbili: Utenzi wa *Fumo Liyongo* uliokusanywa na kuhaririwa na Mohamed Kijumwa na utenzi wa *Al- Inkishafi* ulioandikwa na Seyyid Bin Nassir. Isitoshe, maudhui yanayopatikana katika ushairi wake Muyaka bin Haji yataangaziwa. Lengo kuu hapa ni kuonyesha kuwa ijapokuwa watunzi hawa waliishi katika nyakati tofauti, tungo zao zilifanana kwa kiwango kikubwa kimuundo na kimaudhui isipokuwa zile za Muyaka ambaye alitaka kujitambulisha kama msanii asiyeegemea sana kaida na desturi za ushairi wa enzi yake.

1.1 Mianzo ya Tendi

Shariff (1988), Chacha (1992) na Hassan (2018) wanakubaliana kuwa tenzi za kale zilianza kutaja jina la Mwenyezi Mungu, yaani, Bi-isimi-lahi (Kwa jina la Mungu). Watunzi wa tenzi hizi walimshukuru Mola kwa kuwapa uwezo wa kutunga tenzi zao. Hii ilikuwa njia mojawapo ya kutambua uwezo mkubwa au kudura yake Rabana au Manani kinyume na udhaifu wake mwanadamu. Hata hivyo, tofauti na washairi wa hapo awali Muyaka bin Haji hakuegemea sana sifa za kidini katika maudhui yake wala kuanza utungo wake kwa njia hii. Pengine Muyaka alifanya hivyo kwa kutaka kuwa tofauti na wenzake. Inawezekana kuwa kule kutaka kutofautiana na watunzi wenzake ndiyo mojawapo ya sababu kuu zilizomfanya kulaumiwa kuwa alitoa ushairi misikitini na kuupeleka sokoni. Hii inatokana na sababu kuwa hakuzingatia tu maudhui ya dini ya Kiislamu bali pia masuala mengine yaliyohusu maisha ya kawaida ya watu. Baadhi ya maudhui aliyoyaangazia ni kama vile: mapenzi na ndoa, elimu, uchumi, uzalendo na vita, usaliti, utamaduni, dini, magonjwa na kifo.

Hata hivyo sio kweli kudai kuwa Muyaka hakuwahi kabisa kutaja jina la Mungu

katika mianzo ya tungo zake. Ukweli ni kwamba alifanya hivyo katika baadhi ya mashairi yake ijapokuwa hakuwa na mazoea ya kufanya hivyo. Mifano ni kama ifuatavyo:

*Ilahi wa Maulaya Sayyidiwa Sayyidahu
Naomba hinyenyekea, ya rabbi afuwahu
Mawe ngwatubaidia yaliyo na ikrahu
Faqadarnahu, fa nii malqadinura (1979: 188)*

Tafsiri kutoka Kikae na Kiarabu hadi lugha sanifu:

*Ewe Mungu, Bwana wangu na Bwana wake,
Naomba kwa unyeyekevu, ewe Mungu umponye
Mungu twepushie maovu, mabaya ayanayotudhuru
Ni sisi tuombao, wakuu kati ya wale waombao.
(Tafsiri yetu)*

Hali ya tenzi kuanza kwa kutaja jina la Mola inabainika katika utendi wa Liyongo. Katika utendi huu, mtunzi anaanza kwa maneno ‘Bismillahi nabutadi’ yaani kwa jina la Mola nitanguliza. Aidha, anamuomba Mungu ampe uwezo wa kutunga hadithi ya Liyongo ili waja wafahamu (ubeti wa kwanza). Hali kadhalika, utendi huu pia unianza kwa kutaja jina la mtume Muhammadi. Hali hii inaoana na kauli ya Shariff (1988) anapoeleza kuwa tenzi za kale huweza kuanza kwa kumsalia mtume. Mtunzi anaeleza hivi:

*Bismillahi nabutadi
Kwa ina la Muhammadi
Niandike auladi
Nyuma watakaokuya (ubeti wa kwanza)*

Kwa upande mwingine, Utenzi wa Al-Inkishafi pia unatangulia kwa kutaja jina la Mungu. Mtunzi anatanguliza kwa kumwomba Rabana ampe neema. Aidha, anatambua uwezo wa Mola kwani ni Mungu tu ndiye anayekidhi mahitaji ya wanadamu (ubeti wa tano). Katika ubeti wa kwanza wa shairi hili mtunzi anaeleza hivi:

*Bismillahi naikadimu
Hali ya kutunga hino nudhumu;
Na ar- Rahmani kiirasimu,
Basi ar- Rahimu nyuma ikaye*

Kutokana na haya, imebainika kuwa tenzi hizi mbili zinaanza kwa namna maalum yaani kutaja jina la Mola. Japo tenzi hizi zimeandikwa na watu wa nyakati tofauti na mazingira tofauti, zina maumbo yanayofanana. Ndiposa, Frye (1982) kuwa kazi za fasihi huwa na sura maalum zinazozitambulisha. Aidha, Frye (1982) anaongezea kwa kusema kuwa tofauti

za kimazingira haziathiri maumbo ya kazi za fasihi. Hali hii inaoana na kauli ya Wamitila (2002) kuwa tenzi za kale zina mitindo inayofanana na fasihi simulizi yaani fomula sawia za utangulizi na mwisho wa utungaji, mgogoro wa msuko unaokaribiana na matumizi ya lahaja. Aidha, Beja na Adulrahman (2017) wanaongezea kwa kueleza kuwa watunzi hawa walitaja majina yao. Aidha, wanaongezea kuwa majina kama vile: taqarabu, bismillahi, habibu na sahabaze yana asili ya Kiarabu. Wanatoa mfano huu katika utenzi wa Mwanakupona:

*Ukisa kutaqarabu
Bismillahi kutubu
Umsalie Habibu
Na sahabaze pamoya (ubeti wa nne)*

1.2 Uhitimishaji wa Tendi

Hassan (Tasnifu ya Chuo Kikuu Cha Dodoma: Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili) (2018) anaeleza kuwa tenzi huisha kwa kumshukuru Mola. Watunzi walimshukuru Mungu kwa sababu walilelewa katika mazingira ya kidini. Ndiposa, Mlaga (2017) anabaini kuwa mawazo kuhusu mwenyezi Mungu yataendelea kujitokeza katika kazi mbalimbali za watunzi ambao wamelelewa katika misingi ya kidini. Mawazo kuhusu Mola yanajitokeza katika baadhi ya tenzi kwani watunzi wengi walimshukuru Mungu na kumuomba baraka. Mfano ni utenzi wa Al-Inkishafi ambao unahitimishwa kwa muundo huu. Mtunzi anamuomba Mola awajaliye na ampe rehema mwenye kutunga. Anaeleza hivi:

*Sasa takhitimu tatia tama,
Atako fuata na kuyandama,
Tapata khatima na mwisho mwema
Rabbi, naomba, tujaaliye (ubeti wa 78).*

*Rabbi, mrahamu mwenye kutunga,
Na mezokhitimu, mja malenga.
Sala na salamu ni zao kinga.
Rabbi takabali ziwashukiye (ubeti wa 79).*

Imebainika kuwa tenzi hizi za kale zilikuwa zinakamilika kwa waandishi wao kutambua uwezo wa Mola. Hii ni kwa sababu watunzi hawa wote waliomuomba Mungu awape haja zao ikiwemo neema na baraka. Ndiposa, Sengo (2009) anaeleza kuwa katika kazi za fasihi wema haukunasibishwa na jamii au mtu binafsi bali ulinasibishwa na Mwenyezi Mungu. Kwa mujibu wa nadharia ya ukae, kazi bora ilifaa kuanza na kuisha kwa kutaja jina la Mwenyezi Mungu na kumshukuru.

Sifa nyingine muhimu katika mahitimisho ya tenzi za kale ilikuwa ni mtunzi kujitambulisha nasaba yake na pengine hata kueleza uwezo wa nasaba yake katika sanaa ya utunzi wa tungo za kishairi. Mfano ni utenzi wa Mwana Kupona. Katika utenzi huu mtunzi anajitambulisha. Aidha, anaeleza kuwa ni mjane na amezaliwa Pate. Anaeleza

hivi:

*Mwenye kutunga nudhumu
Ni gharibu mwenye hamu
Na ubora wa ithimu
Rabbi tanghufiria (ubeti wa 97)*

*Ina lake mufahamu
Ni mtaraji Karimu
Mwanakupona Mshamu
Pate alikozaliwa (ubeti wa 98)*

Hata hivyo, sifa hii ya kujitambulisha haijitokezi katika tenzi za Liyongo na Al- Inkishafi. Katika utenzi wa Liyongo mtunzi anahitimisha tu kwa kumuomba Mola baraka. Anahitimisha hivi:

*Tumeziya kukhitimu
Hapo ndio wasalamu
Ilahi tatukirimu
Kwa baraka na afiya (ubeti wa 228).*

Kwa upande mwingine, utenzi wa Al- Inkishafi unakamilika kwa kuomba neema kutoka kwa Mola na kuungama kuwa atakayefuata mawaidha yake atapata mwisho mwema. Aidha, mtunzi huyu hajitambulishi wazi kwa majina yake wala kutambua nasaba yake. Anaeleza hivi:

*Sasa takhitimu tatia tama,
Atako fuata na kuyandama,
Tapata khatima na mwisho mwema.
Rabbi, naomba, tujaaliye (ubeti wa 78).*

*Rabbi, mrahamu mwenye kutunga,
Na mezokhitimu, mja malenga.
Sala na salamu zao kinga
Rabbi takabali ziwashukiye (ubeti wa 79).*

1.3 Lugha ya Tenzi za Kale

Ni dhahiri kwamba watunzi wa ushairi na tenzi za kale walitegemea sana lahaja za nyumbani alikozaliwa na kukulia mshairi. Pengine watunzi hawa walifanya hivi ili kuwafikia wasomaji wa kazi zao waliotoka katika janibu zao. Watunzi wa tungo za kale walizingatia sana lahaja zilizokuwa maarufu katika matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kila siku na pia kama lugha ya usomi. Ni dhahiri wote walitilia mkazo matumizi ya Kiarabu ambayo ilikuwa lugha kuu ya usomi wakati huo. Hii ndiyo iliyokuwa lugha ya tabaka la “Wangwana”, yaani wasomi

ambao walikuwa Makadhi, Maimamu na Maalimu au wafundishaji wa dini ya Kiislamu.

Mtunzi wa Utenzi wa Liyongo, ambaye ni Fumo Liyongo, anayekisiwa kuwa aliishi kati ya Karne ya 12 na 13, aliegemea sana lahaja ya kikae au Kingozi, lugha asilia ya Kiswahili iliyotumika katika eneo la Ozi kati ya Lamu na mto Tana. Hapa ndipo alipozaliwa na kuishi huyu Shujaa Fumo Liyongo. Mifano ya msamiati wa Kingozi aliyoyatumia Liyongo katika utenzi wake ni: neno ‘mkoyo’ linalomaanisha ‘mkojo’, neno ‘lilakuwiliya’ linalomaanisha ‘kutetemeka’, neno ‘kayepuwa’ linalomaanisha ‘akajiepusha’, ‘mayondi’ kumaanisha ‘majonzi’ na ‘kiteko’ kumaanisha ‘kicheko’. Mtunzi anaeleza hivi:

Ghafula kikutoleya
Mkoyo hukupoteya
Tapo likakuwiliya
Ukatapa na kuliya (ubeti wa 14).

Liyongo akatawambuwa
Huzengea kuuwawa
Pale Pate kayepuwa
Barani akitembeya (ubeti wa 50).

Pia Liyongo alitumia maneno mengi ya Kiarabu kwa vile hii ndiyo iliyokuwa chombo cha usomi na mafunzo ya kidini. Kiarabu pia kilikuwa lugha ya ustaarabu au utamaduni katika wakati huu. Mifano ya maneno ya Kiarabu katika utenzi wa Liyongo ni kama vile: Bismillahi, fakhari na Ilahi. Katika utenzi wa Inkishafi, mtunzi Seyyid Bin Nassir aliegemea sana matumizi ya lahaja ya Kiamu iliyokuwa lugha yake asilia. Vile vile alichangaya na maneno machache ya Kiarabu na pia Kingozi. Anatumia maneno kama vile: ‘dhambi’ linalomaanisha ‘kosa’, ‘Bismillahi’ linalomaanisha ‘kwa jina la Mola’. Aidha, maneno kama ‘fedha’ na ‘dhahabu’ yamekopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Maneno haya hayana visawe. Kinyume na watunzi wenzake, kimsingi, Muyaka alitumia sana lahaja yake ya Kimvita kwa vile ni mzawa wa kisiwani Mombasa. ata hivyo yeyé pia alitia msamaiti kidogo wa Kingozi na Kiarabu ili kujitambulisha na tabaka la juu la wasomi ijapokuwa alikuwa wa kutoka kwenye tabaka la wachochole. Hii hapa mifano ya baadhi ya maneno ya Kimvita kutoka katika mashairi ya Muyaka: ‘tuvundao’ kumaanisha ‘tuvunjao’, ‘ndiswi’ kuashiria ‘ndisi’ na ‘swiswi’ kuashiria ‘sisi’.

1.4 Muundo wa Ubeti wa Utenzi wa Kale

Nzuki (2003) anaeleza kuwa baadhi ya tenzi za kale zilikuwa na beti zenye mishororo minne isiyokamilika. Mfano ni utenzi wa Liyongo. Aidha, anaongezea kuwa tenzi hizo hazikuwa na kibwagizo. Hali hii ilibainika ushairi uliotangulia, hasa, katika tendi za Liyongo, Al-Inkishafi na Mwanakupona. Tenzi hizi zote zina beti zilizo na mishororo minne yaani zina muundo wa tarbia. Aidha, tenzi hizi zina kipande kimoja. Hali kadhalika, tenzi hizi hazina vibwagizo. Kwa upande wa mizani, utenzi wa Al-Inkishafi una mizani kumi na moja katika kila mshororo ilhali utendi wa Liyongo una mizani minane katika baadhi ya mishororo. Aidha, utenzi wa

mwanakupona una mizani minane katika kila mshororo. Hali hii inaonyesha kuwa katika tenzi za kale ilikuwa ni sheria kuwa kila utendi uwe na mizani kati ya minane hadi kumi na moja kwa kila mshororo.

Hata hivyo, japo mashairi ya Muyaka yana mshororo minne, mashairi yake yanaonyesha ubunifu wa hali ya juu ikilinganishwa na tenzi za Kale. Muyaka ametumia mbinu tofauti inayomtofausha na watunzi wa Tenzi za Liyongo na Al- Inkishafi. Mbinu hizi ni kama vile: matumizi ya lugha ya kimafumbo, matumizi ya methali kama anwani ya shairi na urudiaji wa baadhi ya maneno na vifungu katika shairi.

Baadhi ya mashairi ya Muyaka yanayotumia methali kama kichwa ni kama vile: “Kimya kingi kina mshindo mkuu” (uk. 194), “Majuto (ni mjukuu) huja kinyume” (uk. 222) na “Nyumba njema si mlango fungua uingie ndani” (uk. 324). Aidha, mashairi haya yanarudia maneno katika kila mshororo. Mfano ni shairi la “Oa” na shairi la “Moyo”. Katika shairi la “Moyo”, mtunzi anaeleza hivi:

*Moyo wanambia kwamba, jambo la mtu usambe
Moyo wanambia omba, kitu cha siombe
Moyo wanambia ramba, tata ya moto sirambe
Moyo watamani pembe, ilo na ndovu kitwani (Moyo: 96).*

Mfano huu unaonyesha urudiaji wa neno ‘moyo’. Pengine kutokana na mashairi yake Muyaka, ndipo baadhi ya watunzi wa baadaye walianza kutunga mashairi ya bahari ya kikwamba na zivundo. Aidha, utumiaji wa methali kama anwani ya shairi unaweza kuwa umetokana pia na mashairi yake ambapo watunzi wa sasa wanaweza kuwa wamekopa mbinu hii kutoka kwake. Hali kadhalika, katika mashairi ya Muyaka kuna urudiaji wa mshororo wa mwisho wa kila ubeti. Hali hii ni tofauti na tenzi za kale kwani katika tenzi hizo mshororo wa mwisho haurudiwi. Mfano wa shairi la Muyaka linalobainisha urudiaji huu ni shairi la “Mjenga Nyumba Halele”. Aidha, urudiaji huweza pia kujitokeza katika kipande cha shairi. Urudiaji wa aina hii unajitokeza katika shairi la Utavaa nguo gani? Lililopo katika diwani ya Muyaka. Mtunzi anaeleza hivi:

*Nipaka kiberiti na mrututu kashombo
Atie mtanashati, fumo kinbombo
Yii hapa hana bahati, tubu mwana kabobo
Huu shuka haunau robo! Utavaa nguo gani?*

*Ka'tatehe la mkeka au domo la kanda
Hadharani ukafika, usikalie kitanda
Wenzio watakuteka, utamani wa kutenda
Kesho wenzio washinda, utavaa nguo gani? (uk. 280).*

Mfano huu unabainisha urudiaji wa kipande utavaa nguo gani. Hata hivyo, shairi hili linatumia maswali ya balagha. Aidha, kila kipande kina mizani minane. Hali ya kutunga mashairi yenye

maswali ya balagha na mizani minane inapatikana katika tenzi za kale. Mfano ni katika utenzi wa Al- Inkishafi ambapo beti za 31, 32, 33 na 26 zinabainisha matumizi ya maswali ya balagha. Mtunzi anaeleza hivi:

*Suu ulimwengu ututakao,
Emale ni lipi upendeyao?
Hauna dawamu hudumu nao,
Umilikishwapo wautendaye? (ubeti wa 31)*

Ubeti huu umetumia maswali ya balagha. Mtunzi anauliza moyo wake ni kwa nini hautendi jambo jema kila wakati. Isitoshe, imebainika kuwa kuna tenzi zingine zilizo na mizani minane katika kila kipande. Hali hii inabainika katika baadhi ya beti zilizoko katika utenzi wa Liyongo. Mfano wa ubeti wa utenzi wa Liyongo ulio na mizani minane katika kila kipande ni huu:

*Kamtiya kitovuni
Naye ulele kwa t'ani
Achamka hamuoni
Kiyana amekimbiya (ubeti wa 179).*

Kwa upande mwingine, tofauti na tenzi za kale, mashairi ya Muyaka yanatumia mbinu ya pindu. Baadhi ya mashairi yake yanayopindua maneno ni kama vile: “Itakapo kukutana” (uk. 156), “Kifo Ikimbizwa Funza” (uk. 172) na Tusambiane uwongo (uk. 220). Katika shairi la “Itakapo kukutana” mtunzi anapindua maneno ‘Ai pato na mpema’ hadi ‘Ai mpema na pato’. Mtunzi anaeleza hivi:

*Simba ndume na wambuji, sikizani t'atongo
Nakotela vitongoji, na safari za mashua
Leo nakumbuka mbiji, ya kutweka na kutua
Ai pato na mpema, itakapo kukutana*

*Ai mpema na pato, lipato mtu kukua
Angawa mwana mtoto wa kutushika kachema (uk. 156).*

Shairi hili linabainisha matumizi ya mbinu ya pindu. Hata hivyo, ubeti huu unaonyesha urari wa vina vya ndani isipokuwa kina cha kati cha mshororo wa mwisho. Hali hii pia inajitokeza katika tenzi za Liyongo na Al- Inkishafi. Katika utenzi wa Al- Inkishafi mtunzi anaeleza hivi:

*Bismillahi naikadimu
Hali ya kutunga hino nudhumu;
Na ar- Rahmani kiirasimu,
Basi ar-Rahimi nyuma ikaye (ubeti wa kwanza).*

1.5 Maudhui ya wema na uovu

Chacha (1992) anaeleza kuwa matendo ya binadamu huathiriwa na Imani walionayo kwa Mwenyezi Mungu. Hichens (1972), Shahid (1980) na Mulokozi (1999) wanakubaliana kuwa tenzi za kale zimesheheni maudhui ya kidini hasa dini ya kiislamu. Dini hii iliwaathiri baadhi ya watunzi wa tenzi za kale kiasi kuwa walisawiri maudhui ya wema na uovu kwa misingi ya kiislamu. Kwao wema ulituzwa ilhali uovu uliadhibiwa.

Katika utenzi wa Mwanakupona mtunzi anatuonyesha faida ya kuwa mtu mwema. Mtunzi anamhimiza mwanawe ashike dini, awe na adabu, awe mnyenyekevu, aheshimu mume na wanajamii wote, aepuke umbeya na aheshimu Mungu. Kulingana naye, matendo haya mema yatamuepushia dhiki duniani na akhera (ubeti wa 95). Aidha, anaeleza kuwa kutokana na kutii mume wako mwanamke huheshimiwa (ubeti wa 96). Hali kadhalika, anamuomba Mungu amuepushe na uovu ili aende peponi na awe miongoni mwa watu wema (ubeti wa 88 na 89). Anaongeza kuwa kumtii mume ina baraka kwani ni yeye ataamua ikiwa mkewe ataenda motoni au peponi (ubeti wa 26 na 27).

Isitoshe, utendi wa Liyongo unaeleza jinsi mwana wa Liyongo aliadhibiwa kutokana na uovu wake. Anamuua Liyongo kwa kumdunga kwa sindano ya shaba kitovuni mwake. Alifanya hivi kwa sababu ya tamaa ya kuoia binti wa mfalme. Mtunzi anaeleza kuwa mwanawe Liyongo alivuliwa nguo zake na akachukiwa na watu (ubeti wa 216). Aidha, mamamkwe wake alimiyima chakula (ubeti 222). Hatimaye, mwanawe Liyongo anadhoofika kiasia (ubeti wa 223).

Kwa upande mwingine, utenzi wa Al-Inkishafi unaelimisha watu na kuwaonya dhidhi ya matendo maovu. Mtunzi anaanza kwa kuonya moyo wake dhidhi ya matendo maovu ikiwemo kuwa na tamaa ya mali (ubeti wa 12 na ubeti wa 13). Aidha, anatueleza kuhusu waja walioishi maisha ya anasa na kisha kuaga dunia ili tujifunze. Anatueleza kuwa Mola humlipa mtu sawia na matendo yake kwani wanaowadhulumu wengine huadhibiwa huku wadhulumiwa wakituzwa (ubeti wa 69, 70, 71 na 72). Isitoshe, anatueleza kuhusu aina za moto ambazo watendao maovu watatupwa ndani. Hatimaye, anaeleza kuwa atakayefuata maonyo yake atapata mwisho mwema (ubeti wa 78).

1.6 Maudhui ya dini

Beja na Abdulrahman (2017) wanaeleza kuwa baadhi ya tenzi ikiwemo Mwanakupona na Al-Inkishafi zilichota maandishi ya Kuran tukufu na Sunnah. Aidha, wanaongezea kuwa tenzi hizi zilitumiwa kama chombo cha kuhubiria dini ya kiislamu. Katika utenzi wa Al-Inkishafi maudhui ya dini yanajitokeza. Utungo huu unaeleza kuhusu aina za moto zilizoko jehanamu na umuhimu wa kutubu. Aidha, mwandishi anaonya moyo wake dhidhi ya uovu. Hali kadhalika, anaanza ubeti wake wa kwanza kwa jina la Mwenyezi Mungu. Mtunzi ana matumaini kuwa akitubu ataenda peponi.

Utendi wa Liyongo unaanza pia kwa jina la Mwenyezi Mungu. Aidha, mtunzi anamalizia kwa kumshukuru Mola. Tenzi hizi zinaonyesha kuwa tenzi za kale ziliangazia sana dini. Watunzi wa tenzi hizi walitawaliwa na imani ya kidini katika kutunga kazi zao. Kinyume na wenzake waliotunda tenzi, Muyaka hakutaja maudhui ya kidini moja kwa moja. Hata hivyo, si kweli kudai kuwa Muyaka alipuuza dini kabisa katika kazi yake. Kwa

mfano katika mashairi haya mawili, Muyaka anasisitiza umuhimu wa kumuomba Mola na Kuzingatia mafunzo yake.

Katika shairi la Mke wa Risasi (uk. 300) Muyaka anamsuta mtu mwengine kwa kutaka uhusiano wa kimapenzi na mke wa marehemu Risasi aliyekuwa katika eda. Kulingana na Imani ya dini ya kiislamu, mjane akiwa katika eda hatakikani kuolewa wala kujiingiza katika shughuli za mapenzi. Wakati wa eda unaashiria wakati ambao mwanamke anajifunika gubigubi kwa nguo nyeupe au nyeusi anapofiwa na mumewe. Mwanamke huyu hujifunika hivi kwa miezi minne na siku kumi na hakubaliwi kuonana na yeyote isipokuwa jamaa wake. Mfano mwingine ni shairi la Moliwa Loke (uk. 123). Shairi hili lilitungwa wakati wapiganaji wa Mombasa waliposhindwa vitani na wanajeshi wa Lamu huko Pate. Meli yao ilivamiwa na ikaanza kuzama. Kutokana na hali hii, wanajeshi wa Mombasa waliuliza Muyaka awape ushauri. Ndipo Muyaka aliomba Mola ili awaondoshee janga hili. Maombi yake yalijibiwa kwani waliwasili salama salimini. Mashairi mengine katika mashairi ya Muyaka yanayosheheni maudhui ya kidini ni kama vile: Shairi la Kongowea Yaungua (uk. 202), Kwa-Mwana kwa Heri (uk. 108), Harusi ya bwana Muyaka (uk. 278) na Kiwi Heri Kupata (uk. 214)

1.7 Maadili na Wosia

Kulinga na Wafula na Njogu (2007) ukae ni wakati maalumu ambapo misingi ya kazi za Sanaa huwekwa na kukubalika kuwa vipimo bora kwa kazi nyingine. Aidha, Wafula na Njogu (2007) wanaongezea kuwa maudhui ya kuwaasa wanajmii ni kikale katika kazi ya fasihi. Kazi hizi ikiwemo tenzi za kale ziliwapa wosia vijana ili wabadilishe mwenendo wao. Katika utenzi wa Mwanakupona, mwandishi ananua kumpa wosia mwanawe. Katika ubeti wa 92 mtunzi anaeleza hivi:

*Na sababu ya kutunga
Si shairi si malenga
Nina kijana muinga
Napenda kumuusia (ubeti wa 92 uk. 138).*

Mfano huu unaonyesha dhamira ya mtunzi. Anaeleza kuwa sababu yake ya kutunga ni kuwa ana kijana mjinga angependa kumpa mawaidha. Aidha, mtunzi hakulenga tu kumpa mwanawe pekee mawaidha bali vijana wote. Anaeleza hivi:

*Someni nyute huramu
Maana muyafahamu
Musitukue laumu
Mbee za mola Jalia (ubeti wa 94).*

*Somani mite ya nganu (vijana/ wachanga)
Mutii waume zenu
Musipatwe na zitunu
Za akhera na dunia (ubeti wa 95).*

Beti hizi katika Utenzi wa Mwanakupona zinabainisha kuwa mtunzi alilenga kuwapa wosia pia vijana wengine. Anawahimiza wanawake wote wasome utungo huu ili wasilaumiwe na Mola siku ya hukumu. Aidha, anawaambia wasome utungo ili wawatii waume ili wasipatwe na dhiki duniani na akhera. Kwa upande mwingine, Utenzi wa Al-Inkishafi haulengi tu kuasa hadhira pekee bali pia mtunzi mwenyewe. Mtunzi anaanza kwa kutupa ahadi kuwa atatutungia kidani cha lulu. Anaeleza hivi:

*Makusudi yangu ya kudhamiri,
Nda kutunga koja kilidawiri,
Mivazi ya duri ikinawiri,
Mikinda ya lulu nyuma nitiye (ubeti wa 7 uk. 83).*

Mfano huu unabainisha kuwa mtunzi alilenga kutupa ‘vitu vya thamani’. Ndiposa anatumia neno ‘koja’ yaani maua. Maneno ya mafunzo na mawaidha anayotoa mtunzi yana thamani kuu kama vile vito vya lulu na kadhalika. Baadaye, inabainika mwishoni mwa utenzi kwani baada ya kusoma utenzi wenyewe tunasawishika kubadilisha mienendo yetu. Aidha, tunasawishika kuwa mtunzi ametuzindua kuhusu masuala fulani ikiwemo utajiri. Ndiposa, anatusawiria picha ya waja waliowadhulumu watu kwa sababu ya utajiri wao na hatimaye wakaaga dunia. Anaeleza kuwa baada ya kifo ni hukumu.

Sifa mojawapo muhimu ni matumizi ya mbinu ya “uzungumzi nafsia” ambapo mtunzi anaongea na moyo wake kama vile moyo wake anauchukulia kuwa “hadhira” inayomsikiliza. Hata hivyo, mtunzi hakulenga tu kuwapa mawaidha hadhira yake bali pia kujiasa mwenyewe. Mtunzi anaeleza hivi:

*Kimakwe kuisa dibaji yangu,
Penda kuuonya na moyo wangu,
Utetwe ni hawa ya ulimwengu,
Hila za Rajimi ziughuriye (ubeti wa 10 uk. 84).*

Ubeti huu unabainisha jinsi mtunzi anauonya moyo wake dhidhi ya ‘hawa’ yaani tamaa. Aidha, anaongezea kuwa ujanja wa ibilisi usidanganye moyo wake. Mtunzi anauasa moyo wake uepuke tamaa ili aepukane na maovu ya dunia.

Kwa upande mwingine, maudhui ya wosia yanajitokeza katika mashairi ya Muyaka. Hata hivyo, Muyaka hakudhamiria tu kuifunza jamii kuhusu umuhimu wa elimu ya jamii bali pia elimu ya shuleni. Katika shairi la Kisa ni Halali? (uk. 312) anawashauri wenyeji wasome ili wapate majibu. Anatumia maneno ‘vifunueni vitabu’ kuashiria kusoma vitabu au kujielimisha. Anaeleza hivi:

*‘Kwani sikupata jibu, kwa kuchelea makosa
Vifunueni vitabu, nyote wasomi darasa!
Munipe njema jawabu, mpatela kufuasa
Munambie “Huyu K’asa, ni halali, ni haramu” (uk. 312).*

1.8 Maudhui ya kifo

Maudhui ya kifo yanajitokeza katika tenzi za kale. Utendi wa Liyongo unasawiri kifo kama jambo linalosababishwa na udhaifu wa mwanadamu. Mtunzi anaeleza kuwa Liyongo ndiye alisababisha kifo chake. Hii ni kwa sababu licha ya kujua kuwa mwanawe anataka kumuua anamuambia siri ya nguvu yake. Anamueleza kuwa kinachoweza kumuua ni msumari wa shaba (ubeti wa 43). Aidha, mwanawe Liyongo anaaga hatimaye. Anakufa kwa sababu alifanya makossa kwa kumuua Liyongo. Anapoambiwa kuwa Liyongo ameaga anacheka badala ya kulia. Hatimaye, mfalme anamyanganya kila kitu mwanawe Liyongo na kumfukuza. Mwishowe, mwanawe Liyongo anaaga dunia kutokana na maradhi yasiyopona. Mtunzi anaeleza hivi:

*Siku chache kitimiya
maradhi yakamngiya
yasiyomuondokeya
naye kisa kaifiya (ub. Wa 223 uk. 56).*

Mfano huu unabainisha jinsi ambavyo mwana wa Liyongo alivyoaga dunia kutokana na maradhi. Kwa upande mwingine, maudhui ya kifo yameangaziwa katika utenzi wa Al-Inkishafi. Kulingana na mtunzi wa utenzi huu, kifo humpata mtu yeyote awe ametenda makosa au la. Mtunzi anaeleza kuhusu watu mbalimbali walioishi maisha ya kifahari na hatimaye wakakufa. Waja anaowaangazia ni kama vile: Ali bin Nasir, Abubakari, mashujaa wa Pate na mtume Suleimani. Mtunzi anaeleza hivi:

*“Namua na huyo menidhilimu,
kwa hukumu yako ilio nyumu!”
Mungu Jabari akahukumu,
“Amtendeleo amlipiye!” (ub. wa 69 uk. Wa 98).*

Ubeti huu unabainisha kuwa Mungu humlipa mtu kutokana na matendo yake duniani. Waliotenda mema wakiwa duniani hupewa timbe, dhahabu na fedha ilhali waliowadhulumu wengine hutiwa motoni. Kwa upande mwingine, Muyaka pia aliangazia maudhui ya kifo. Katika mashairi yake anaonyesha kuwa kifo ni tukio lisiloepukika. Hali hii inabainika katika shairi la “Kifo kikimbizwa Funza” (uk. 172). Muyaka anaeleza:

*Kifo kikimbizwa Funza chawekwa mahali gani
Sifakie kifunza, ukakitia shimoni,
Ndanini kujjumiza, kujitia mashakani?
Wapeni mabaniani, mahali wafakiweka (uk. 172).*

Hali kadhalika, mashairi ya Muyaka yanaangazia maudhui ya magonjwa. Hali hii ni sawia na utenzi wa Liyongo ambapo mtunzi ameangazia maudhui ya magonjwa. Mashairi ya Muyaka yaliyoangazia maudhui ya magonjwa ni kama vile: “Kongowea Yaungua” (uk.

202), “Itakapo Kukulana” (uk. 156) na “Aha!” (uk. 188). Aidha, Inabainika kuwa wakati wa kutunga mashairi yake Muyaka alikuwa mgonjwa sana. Hali hii ni sawia na utenzi wa Mwanakupona ambapo Mwanakupona alitunga utenzi huu akiwa na maradhi ya tumbo. Mfano wa shairi linalothibitisha kuwa Muyaka alikuwa ni mgonjwa ni shairi la “Aha!”. Katika shairi hilo mtunzi anaeleza hivi:

*Aha! Sengambile, Aha! Ndwele yaniuma
Aha! N’ambe, sina siha, muwili wangu mzima
Aha! Kutoona raha, ndipo aha! Nikasema
Aha! Sambile kwa wema, nasema kwa ndwele sii*

1.9 Maudhui ya Vita na Uzalendo

Maudhui ya vita yanajitokeza katika mashairi ya Muyaka na tenzi za kale. Katika utenzi wa Liyongo, mtunzi anasawiri vita baina ya Liyongo na wasanye. Wasanye na wadhallo walijaribu kumuua Liyongo lakini wakashindwa. Hata hivyo, mfalme anamshawishi mwanawe Liyongo atafute siri ya nguvu ya Liyongo. Mwanawe Liyongo anaonelea kwa kumuua Liyongo atakuwa ameonyesha uzalendo wa hali ya juu. Hata hivyo, Liyongo anapoaga dunia mwanawe Liyongo anaadhibiwa badala ya kutuzwa.

Kwa upande mwingine, mashairi ya Muyaka pia yanaonyesha vita. Hata hivyo, Muyaka hakujiegemeza tu katika kusawiri tu vita baina ya wenyeji bali pia vita kati ya wenyeji na wakoloni. Anafanya hivi ili kuonyesha matukio ya kihistoria ambapo wenyeji walipinga kutawaliwa na wakoloni. Mifano ya mashairi ni kama vile: shairi la “Vikija Mtaviweza” (uk. 133-134), “Kongowea Ja Mvumo” (uk. 146) na “Mjenga Nyumba Halali” (uk. 124). Katika shairi la “Vikija Mtaviweza” anaeleza jinsi wenyeji walipojitayarisha kukabiliana na wakoloni. Anaeleza hivi:

*Kongowea haitui, hamtaki kuituza
Mshishile uadui, kutaka kupinduzwa
Ndipo ikashika kawi, kutaka wafanikize
Vikija mtaviweza, au mwatakia mabo? (uk. 133-134).*

Hitimisho

Makala haya yameelezea miundo na maudhui yanayopatikana katika tenzi mbili za kale. Tenzi hizi ni: utenzi wa Liyongo na utenzi wa Al- Inkishafi. Kwa upande mwingine, tenzi hizi zimelinganishwa na kulinganuliwa na mashairi ya Muyaka bin Haji. Imebainika kuwa kuna sifa chache za kimuundo za tenzi zinazofanana na zile za mashairi ya Muyaka. Sifa hizi ni urari wa vina, matumizi ya maswali ya balagha, idadi ya mishororo katika kila ubeti na matumizi ya lahaja. Aidha, utenzi wa Liyongo una mizani minane katika kila kipande cha mishororo kama ilivyo mashairi ya Muyaka. Isitoshe, tenzi hizi na mashairi ya Muyaka yanasheheni maudhui ya dini, wosia, kifo na wema na uovu. Hata hivyo, kuna sifa kadhaa zinazotofautisha mashairi ya Muyaka na tenzi za kale. Katika tenzi za kale, kuna mianzo na miishio maalum. Tenzi hizi zilianza kwa kutaja jina la Mola na kuishia kwa kumshukuru

Mola. Hali hii ni kinyume na Mashairi ya Muyaka kwani mashairi mengi yake hayaanzi hivi. Hata hivyo, mashairi mengi ya Muyaka hayaanzi kwa mtindo huu. Kuna mashairi ya Muyaka machache yanayoanza kwa mtindo huu wa kutaja jina la Mola. Inaonekana kuwa Muyaka alifanya hivi, ili kujitambulisha kama msanii. Ndiposa, anapea maudhui mengine kipaumbele kama vile elimu, siasa, biashara, uzalendo na vita. Yawezekana kuwa mtunzi huyu alionelea kuwa ni vyema pia kuyaangazia masuala mengine yanayoathiri jamii na sio kujiegemeza tu katika dini kama kigezo cha kupimia kazi bora. Ndiposa, anaangazia masuala ya dini katika mashairi machache kama vile: Mkewe Risasi (uk. 300), Moliwa Loke (uk. 123), Kongowea Yaungua (uk. 202) na Kiwi Heri Kupata (uk. 214). Muyaka anasawiri vita baina ya wenyeji na wakoloni. Hali hii ni tofauti na tenzi tulizojadili.

Miundo inayotumika katika mashairi ya Muyaka pia ni tofauti na zile za tenzi za kale. Mashairi yake Muyaka yamesheheni methali kama anwani ya shairi, urudiaji wa maneno, vipande na mishororo. Pengine, kutokana na mashairi yake ndipo watunzi wa sasa wamejifunza jinsi ya kutunga mashairi ya kikwamba, pindu na zivindo. Ndiposa, wengi wanamuona kama ‘baba wa mashairi ya kiarudhi’. Inaonekana kuwa Muyaka alitumia muundo tofauti ya ushairi ili ajitofautishe na wenzake. Aidha, pengine alitaka kutambulika ili wengine watakaofuata wamuige.

Funding: This research has no external funding. It has been funded by the autor.

Conflict of Interest: No conflict of interest applies.

Disclaimer Statement: This journal article has not been submitted to any journal for publication.

Author Bionote:

Dr Jesse Murithi (PHD) is a lecturer at Kenyatta University. He teaches Kiswahili literature with special research interests in oral literature, comparative literature and theories of literary criticism. Dr Murithi has published over twenty articles in peer reviewed journals with high impact factor. Mr Misigo Daniel Mwanzu is a Kiswahili and Religious studies teacher at Magumu High School in Nyandarua county. He is also a masters student at Kenyatta University pursuing Masters in Kiswahili.

Authorship and Level of Contribution:

This article was authored by Dr. Jesse Murithi and Misigo Daniel with equal level of contribution.

Marejeleo

- Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 20th Century Popular Poetry*. Nairobi: OUP.
- Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi*. Dar- es- Salaam. Dar- es- Salaam University Press.
- Frye, N. (1957). *Anatomy of Criticism: Four Essays*. New Jersey: Princeton University Press.
- Frye, N. (1982). *The Great Code: The Bible and Literature* (vol. 19). Toronto: University of Toronto Press.
- Hassan, R. H. (2018). *Ujaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Tungizi za Mnyangatwa na Diwani ya Midulu*. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Dodoma, Dodoma, Tanzania.
- Karisa, B. S. na Mwinyifaki, A. (2017) 'Iktibasi' katika Tenzi za Mwanakupona na Al- Inkishafi. *Kioo cha Lugha*, 11(1).
- Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Karne ya 21*. Dar-es- Salaam. Dar- es-Salaam University Press.
- Mulokozi, M. M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar- es- Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Sengo, T. S. Y. (2009). *Tungizi za Mnyagatwa*. Dar- es- Salaam: Al- Amin Education and Research Academy.
- Shahid, I. (1980). 'Arabic Literature' in Holt (1991). *Cambridge History of Islamic Vol. 2B*. Cambridge University Press, 657- 671
- Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu*. Trenton: The Red Sea Press.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.